# MASOMO YA BIBLIA


## KWA

## WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

**Mwaka wa Kwanza**

**Kitabu cha Nne**



## YESU ANIPENDA
## (JESUS LOVES ME)

Key $E^b$

```
Yesu Anipenda,       /s :m :s :s / .d' :-/s :m
Yesu Anipenda,          :d :d/m.r :-l
Kweli Anipenda,      /s :m :s :s l/.d' :- .l/s .d
Mungu Amesema.          :m/.r/d :-//
```

## JESUS LOVES THE LITTLE CHILDREN OF THE WORLD

Jesus loves the little children,
All the children of the world.
Red and yellow, black and white,
They are precious in his sight;
Jesus loves the little children of the world.

## USIKU WALIPOKETI
## (WHILE SHEPHERDS WATCHED THEIR FLOCKS)

Usiku walipoketi wachunga wa kondoo,
Malaika alishuka kwa nuru ya mbingu,
Kwa nuru ya mbingu,
Kwa nuru ya mbingu.

## NJIA YA FURAHA
## (THE HAPPY WAY)

Key D

```
Na mpendaane,           /m .m :m .m/m :d/s .s :s .s/l :s/
Na mpendaane,           /d' :t.l / s .l :s .f/m .m :s .m/
Hii ni njia ya Furaha,  /r :d//
Na mpendaane.
```

Na msaidiane,
Na msaidiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na msaidiane.

Na mshirikiane,
Na mshirikiane,
Hii ni njia ya furaha,
Na mshirikiane.



# MASOMO YA BIBLIA
## KWA
## WATOTO WA MIAKA 4-6

## MWALIMU

**Mwaka wa Kwanza** **Kitabu cha Nne**

B1 - 4Ts

Used by permission of International Publications Services

© Copyright 1986
Baptist Publications House
All rights reserved

Published and Printed by
BAPTIST PUBLICATIONS HOUSE
Thika Road, Ruaraka
BOX 30370, NAIROBI

## HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUJITAYARISHA KUFUNDISHA

Hatua ya 1: Jitayarishe mwenyewe kwa maombi.

Hatua ya 2: Soma somo lote.

Hatua ya 3: Soma kuhusu mkazo wa somo na ufikirie jinsi unaweza kutimiza lengo hilo.

Hatua ya 4: Soma maandiko ya Biblia.

Hatua ya 5: Jifunze kusimulia hadithi kwa watoto.

Hatua ya 6: Jifunze kifungu cha Kukumbuka.

Hatua ya 7: Jifunze kuimba nyimbo zilizopendekezwa.

Hatua ya 8: Jifunze mpango wa kufundisha somo.

Hatua ya 9: Fika mapema Jumapili na utayarishe mahali pa kukutania.

## HATUA ZA KUFUATA DARASANI MWAKO KILA JUMAPILI

Hatua ya 1: Fika mapema; na utayarishe mahali pa kukutania.

Hatua ya 2: Watoto wanapofika:
Mkaribishe kila mmoja, na umwite kwa jina lake.
Pokea sadaka.
Weka alama kwa kitabu cha rekodi.
Andika kila jina la mtoto katika kitabu.

Hatua ya 3: Kulifundisha somo:
Kila siku utatumia nyimbo, wakati wa maombi, vifungu vya Biblia, anza kusimulia hadithi ya Biblia kwa kitendo. Hata hivyo, utaratibu huu waweza kutofautiana; fuata mpango uliopendekezwa kila wiki.

Kila mara wape watoto nafasi ya kujibu maswali unayouliza na kushirikiana katika mawazo yao.

Hatua ya 4: Wakati watoto wanapoondoka:

Ikiwezekana, mpe kila mtoto karatasi ya kupeleka nyumbani ambayo ina picha ya hadithi ya leo.

DOKEZO: Kama watoto hawafahamu nyimbo zote, wafundishe wimbo mpya kila mwezi. Pia, waweza kutumia nyimbo wanazofahamu.

## JINSI YA KUFUNDISHA WIMBO MPYA

1. Imba wimbo wenyewe vizuri na pole pole huku watoto wakiwa wanasikiliza.
2. Baada ya kuuimba tena, waulize watoto una maana gani.
3. Waambie watoto waseme maneno yake baada ya kuyasema.
4. Waambie watoto waimbe pamoja nawe.
5. Rudia wimbo huo huo wakati tofauti mkiwa darasani.
6. Kumbuka kwamba utafundisha maneno yake, sauti na maana yake.

### YESU NI RAFIKI MWEMA (MY BEST FRIEND IS JESUS)

Key $B^b$

Yesu ni rafiki,
Msifuni, msifuni,
Yesu ni rafiki,
Namsifu.

s .m :r .m/d :s/r :s/m :s/
s .m :r .m/d :s/r :s/d :-/

### MSUFUNI BWANA (PRAISE HIM)

Msifuni Bwana, msufuni Bwana,
Enyi watoto wadogo,
Mungu ni upendo, Mungu ni upendo.

### JESUS HELPED THE SICK

Key F

Jesus helped the sick,
Jesus helped the blind;
Every day he went about
Doing something kind.

/m .m :m .f /s :- /
/r .r :r .m /f :- /
/m .m :s .s /f .f :1 /
/s .m :r .m /d :- //

### DUNIA YA MUNGU (GOD'S BEAUTIFUL WORLD)

Key G

Dunia ya Mungu, Dunia ya Mungu
Napenda dunia ya Mungu.
Aliumba kwa mimi, Aiumba kwa wewe,
Napenda dunia ya Mungu.

Dunia ni nzuri; dunia ya Mungu,
Aliniumbia, Aliniumbia,
Napenda dunia ya Mungu.

/s, /s, :m :r /d :- :s, /
/s, :f :m /r :- :s, /
/s, :t, :r /f :s :f /m :- :- /- :- /
/s, /s, :d :r /m :- :s, /
/1, :r :m /f :- :f /
/s :m :d /r :t, :s, / d :- :- /- :- /

### THE BIBLE

I love God's Bible book;
I love its stories true;
They tell me God is wise and good,
And loving too.

### ALITUPENDA NA AKAMTUMA MWANAWE (HE LOVED US AND SENT HIS SON)

Key F

Alitupenda, Alitupenda,
Alitupenda na akamtuma Mwanawe,
Alitupenda, Alitupenda,
Alitupenda na akamtuma Mwanawe.

/s, /s:-:- 1:-:- /1:-:- s:-:- /
/f:m:r f:m:r /r:-:- d:-:s,/
/s:-:- 1:-:- /1:-:- s:-:- /
/f:m:r f:m:r /d:-:- :-: /

## NYIMBO

### NISAIDIE KUWA MWEMA
### (HELP ME TO BE KIND)

Nisaidie kuwa mwema,
Ee Mungu siku yote;
Nisaidie kufanya yale yanipasayo,
Kazini kwangu na michezoni.

```
Key Eb    /s .s :l .s/s .f :m/r :d .r/m :-/
          /s .s :l .s/s .f :m/r .r :m .r/d :-/
```

### LEO TUNAFURAHA
### (WE'RE GLAD TODAY)

Twa furahi leo, twa furahi leo,
Kwa mama zetu twa furahi:
Asante Baba Mungu.

```
Key Ab
/s /m' :- :d /l :- :s /f' :- :t /l :- :- /
   /s :- :l /t :l :s /d' :- :r /m' :- :- /
   /l :- :- /d' :- :- /t :- :- /r' :- :- /
   /r' :- :- /- :- :- /d' :- :- /:- :- /
```

Tumia pia: baba, nyumba, chakula, na kadhalika.

### MARAFIKI
### (FRIENDS)

Marafiki, marafiki,
Sisi tu marafiki,
Kwa kucheza kwa furaha.

```
Key D
/s :l /s .m :d . /
/r .m :f .s /l .t :d' . /
```

### NAPENDA KANISA
### (I LIKE TO GO TO CHURCH)

```
Key G
Na-penda Ka-ni-sa,   : .s,d.r:m.f s:-.s d.r:m.f s:-.3
Na-penda Ka-ni-sa,   :  f.m:r.f m.f:s.l s.f:m.r d: .
```

Na-penda Ka-ni-sa,
Na-penda Nyi-mbo twa-im-ba,
Na-penda Ka-ni-sa.

### JUMAPILI YENYE FURAHA
### (HAPPY SUNDAY MORNING)

Jumapili yenye furaha,
Jumapili yenye furaha,
Husoma Biblia, kuimba na kuomba,
Asubuji hii njema.

```
Key Eb
/m .m :m .f /s :d' /
/l .l :t .l /s :m .s /
/f .m :r .f /m .l :s /
/d' .s :m .f /r :d //
```



## YALIYOMO


Hatua za kufuata katika kujitayarisha kufundisha ........ 2

Hatua za kufuata kila Jumapili darasani mwako ........ 2

**LENGO LA 1: MARAFIKI HUNISAIDIA**

**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto kufahamu kwamba Mungu aliwapangia watu wasaidiane.

Mungu alijua kwamba watu hawangeweza kuishi peke yao. Kwani wao hutegemeana. Tunapaswa kila mara kuisaidia jamaa yetu na marafiki wetu pia.

Watoto wanaweza kusaidiana. Wape watoto nafasi ya kuwasaidia wenzao.

Somo la 40 Chumba cha Elisha ........ 4

Somo la 41 Boazi Mkulima ........ 6

Somo la 42 Marafiki Wanne Wema ........ 8

Somo la 43 Rafiki wa Kipofu ........ 10

**LENGO LA 2: MUNGU ALIUMBA ULIMWENGU MZURI NA WA KUPENDEZA**

**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto kufahamu kwamba Mungu ndiye muumba.

Pia, kumsaidia kila mtoto kuelewa kwamba Mungu alipanga na akauumba ulimwengu.

Somo la 44 Usiku na Mchana ........ 12

Somo la 45 Mvua ........ 14

Somo la 46 Jua ........ 16

Somo la 47 Vitu Vinavyokua ........ 18

Somo la 48 Ulimwengu Mzuri ........ 20

**LENGO LA 3: YESU NDIYE KIPAWA KIKUU CHA MUNGU**

**Kusudi:** Kumwongoza kila mtoto ili afahamu kusudi letu la kuwa na sikukuu ya Krismasi na kufahamu pia kwamba Mungu alimtoa Mwanawe wa pekee kwa sababu anatupenda.

Somo la 49 Malaika Wamtembelea Mariamu ........ 22

Somo la 50 Kuzaliwa Kwa Yesu ........ 24

Somo la 51 Wachungaji na Malaika ........ 26

Somo la 52 Zawadi Za Yesu ........ 28

Nyimbo za Kutumia ........ 30



**Somo la 40**

# CHUMBA CHA ELISHA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu aliwapangia marafiki wasaidiane.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Bwana yu Mwema" (Zaburi 34:8).

Nyimbo:

"Nisaidie kuwa Mwema"
"Leo Ninafuraha"
"Marafiki"
"Napenda Kanisa"

Tumia picha Namba 40

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 2 Wafalme 4:8-10

Vifungu hivi vinaeleza jinsi Mungu alivyomtimizia Elisha mahitaji yake. Mwanamke mmoja wa mji wa Shunemu alishiriki chakula chake na nyumba pamoja na mtumishi huyu wa Mungu. Elisha alimshukuru sana kwa wema huo wake.

Elisha alikuwa nabii wa Mungu. Alikuwa na kazi kubwa sana na pia alifanya miujiza mingi. Alimwokoa mtoto wa mjane mmoja kutoka utumwani (soma 2 Wafalme 4:1-7). Alimponya, Naamani, jemadari wa Shamu, ugonjwa wa Ukoma (soma 2 Wafalme 5). Aliwashauri Waisraeli wakati wa vita vyao na Washami.

Elisha alisafiri hadi mji wa Shunemu mara kwa mara. Akiwa huko, mwanamke mmoja alimkaribisha nyumbani kwake. Akamwambia mumewe, "Naona kama mtu huyu ni mtumishi wa Mungu". Elisha alijulikana kuwa mtu wa Mungu kwa sababu ya matendo yake.

Utataka kuwafundisha watoto kwamba Mungu amewapangia marafiki wasaidiane. Mwanamke huyu alimsaidia Elisha, rafiki yake.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto jinsi rafiki afanyavyo. Sema, "Leo ninafuraha sana kwa sababu ______ (sema jina la kila mtoto) amefika kuhudhuria Shule ya Jumapili."
2. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
3. Sadaka: Waambie watoto kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka mara tu wafikapo darasani.
4. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya kanisa na marafiki.
5. Ita jina la kila mtoto na uweke alama katika kitabu chako kando ya yule aliyehudhuria. Mwambie kila mtoto asimame asikiapo jina lake. Shikaneni mikono katika mviringo.
6. Wimbo: "Napenda Kanisa"



5. Wimbo: "Msifuni Bwana"
6. Uliza, "Je, mtu ye yote aliwatembelea wakati dada au kaka yako alipozaliwa? Walijuaje mmepata mtoto mchanga? Je, marafiki waliowatembelea walikuwa na furaha? Hata Yesu naye alitembelewa na wageni, pia."
7. **Fungua Biblia Yako katika Mathayo 2** na usimulie hadithi ya:

**ZAWADI ZA YESU**

"Hebu njoo uone. Kumetokezea nyota," mamajusi mmoja alisema. Je, inamaanisha nini?"

"Nafikiria inamaanisha kwamba mfalme amezaliwa. Hebu na tuifuate nyota hii. Kwani twaweza kumwona mfalme huyu. Pia, tutampelekea zawadi," mwingine akaongeza.

Mamajusi hao walikuwa na elimu sana. Walijua habari za nyota. Walifahamu kwamba kulikuwa na nyota maalum (angani) mbinguni.

Walianza kujitayarisha kwa safari yao. Wakaweka mizigo na zawadi zao juu ya ngamia. Kila mmoja alibeba zawadi maalum kwa ajili ya mfalme aliyezaliwa. Mmoja wao alibeba dhahabu, mwengine akachukua manukato mazuri ya uvumba na watatu naye alibeba manemane.

Watu hao walisafiri kwa muda mrefu sana kabla ya kufika Yerusalemu. Wakaenda hadi kwa mfalme Herode. Wakamwuliza habari za mfalme aliyezaliwa.

Mfalme Herode alifadhaika sana aliposikia habari hii. Hakujua kuwepo kwa mfalme mwingine. Hatimaye aliwauliza makuhani na waandishi kuhusu habari hii.

"Manabii wamesema kwamba atazaliwa Bethlehemu. Naye atatawala wana wa Israeli," kuhani mmoja akamwambia.

Mfalme Herode hakuhitaji mtawala mwingine. "Nendeni mkatafute habari za mtoto huyu. Mtakapompata, niambieni na mimi. Kwani mani ningependa kumsujudia pia."

Herode alikuwa mtu mkatili. Hakuwa na nia ya kumsujudia Yesu, bali alitaka kumwua tu.

Mamajusi hao waliondoka. Wakaifuata nyota hiyo hadi Bethlehemu. Mwishowe, walimpata Yesu na Mariamu, mama yake. Wakaanguka na kumsujudia. Walimtolea zawadi zao na wakamsifu Mungu kwa kumtuma mfalme mwengine.

Usiku huo huo, malaika aliwatokezea mamajusi hao. Akawaonya kwamba wasirudi kwa Herode wala kumpasha habari hii. Nao walifuata njia nyingine hadi nyumbani kwao.

8. Waonyeshe picha namba 52. Eleza kuhusu mamajusi na sababu iliyowafanya kwenda kumwona Yesu.
9. Omba ukimshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu.
10. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe".
11. Waongoze watoto wajifunze kifungu hiki, "Mshukuruni Bwana" (Zaburi 136:1).
12. Maombi:

Mwalimu: "Kwa ajili ya Yesu aliyezaliwa kama mtoto."

Watoto: "Twakushukuru sana, Mungu".

Mwalimu: "Kwa ajili ya upendo na nyumba tuishimo."

Watoto: "Twakushukuru sana, Mungu."

Mwalimu: "Kwa ajili ya marafiki na upendo wake hapa ulimwenguni."

Watoto: "Twakushukuru sana, Mungu."



Somo la 52

# ZAWADI ZA YESU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Yesu alipewa zawadi.

**Kifungu cha Kukumbuka:**
"Mshukuruni Bwana" (Zaburi 136:1).

Nyimbo:
"Leo Tunafuraha"
"Njia ya Furaha"
"Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"
"Usiku Walipoketi"
"Msifuni Bwana"

Tumia picha Namba 52.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mathayo 2:1-12

Mamajusi walisafiri hadi Bethlehemu wakimtafuta mfalme wa Wayahudi. Walikuwa wakimtafuta Yesu. Walimletea zawadi kwa sababu walimpenda.

Mamajusi walikuwa watu wenye elimu ya nyota. Nyota ngeni kuwa ilimaanisha kwamba mfalme amezaliwa. Walikuwa wakitarajia mtawala mwengine. Mtawala huyo angeleta amani ulimwenguni kwote.

Walibeba zawadi zao waliposafiri hadi kule ilikokuwa nyota hiyo. Walisafiri kwa siku nyingi sana. Pengine walitumia ngamia katika safari hii yao.

Mfalme Herode alikasirika sana wakati mamajusi hao walipofika Yerusalemu na kuuliza habari za mfalme aliyezaliwa. Mungu alijua fikira za Herode. Akawaonya mamajusi hao kutorudi tena kwa Herode. Nao walipitia njia nyingine wakirudi nyumbani kwao.

Nyota ile ambayo mamajusi waliona wakiwa nyumbani kwao, ilionekana tena walipotoka Yerusalemu. Nyota hii iliwaongoza hadi Bethlehemu, mahali alipozaliwa, Yesu.

Mamajusi hao walimsujudia, walipomwona mtoto Yesu. Wakamtolea zawadi zao na kumsifu Mungu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Imbeni, "Leo Tunafuraha", unapowasalimia na kuwakaribisha watoto. Waulize wakwambie lile walilofurahia siku ya leo.
2. Sema, "Mamajusi walimtolea Yesu zawadi. Nasi twaweza kutoa zawadi zetu, pia." Kila mmoja atatakiwa kuja na kuweka sadaka yake katika chombo cha sadaka.
3. Ita jina la kila mtoto. Fanyeni mviringo unapoendeleza kutaja jina la kila mtoto.
4. Mchezo: Watoto wanatakiwa kufanya kile ufanyacho. Sema, "Namshukuru Mungu kwa kunipa miguu. (Inua miguu juu, mmoja baada ya mwingine ukiwa umesimama mahali hapo hapo.)

   Namshukuru Mungu kwa kunipa mikono. (Msalimie mtoto kwa kushikana mikono).

   Namshukuru Mungu kwa kunipa macho. (Shika macho yako.)

   Namshukuru Mungu kwa kunipa masikio. (Shika masikio yako.)

   Namshukuru Mungu kwa kunipa mdomo. (Shika mdomo wako.)

   Uliza, "Je, twawezaje kutumia vitu hivi kwa kumtukuza Mungu?"



7. Uliza, "Je, mama hufanyaje atembelewapo na mgeni?" Ngoja watoto wajibu. "Je, wewe husaidia? Hufanya nini?"

   "Je, umewahi kuwatembelea watu wengine? Ulifanyaje? Je, ulilala huko?" Ngojea watoto waeleze safari walizofanya kwa wenzao.
8. Sema, "Hadithi yetu ya leo inahusu mtu mmoja aliyemtembelea rafiki yake." **Fungua Biblia Yako katika 2 Wafalme 4** na usimulie hadithi ya:

**CHUMBA CHA ELISHA**

"Habari yako, mchungaji Elisha. Waonekana mchovu sana. Je, waweza kuja nyumbani kwetu na upumzike kidogo? Je, utakula pamoja nasi?" Mwanamke mmoja alimwuliza Elisha.

"Asante sana, lakini natakiwa kuendelea na safari," Elisha akamwambia.

"Tafadhali njoo. Tunataka upumzike kabla ya kufika uendako." Mwanamke huyu alimkaribisha mchungaji Elisha nyumbani kwake.

Elisha alikubaliana naye. Alikuwa amechoka sana. Alikuwa ametembea safari ndefu wakati wa jua kali.

Aliingia katika nyumba. Mwanamke huyo pamoja na mumewe waliongea na Elisha. Hata wakampikia chakula.

"Umewahi kufika katika kijiji chetu," mwanamke huyo akamwambia.

"Ndiyo, mimi hutembelea vijiji vingi sana. Hata huwa napita hapa mara kwa mara," Elisha akamwambia.

"Unakaribishwa kuja na kupumzika hapa kwetu iwapo utakuwa safarini."

Mchungaji Elisha aliendelea na safari yake, baada ya kupumzika. Kila mara alipokuwa safarini, aliweza kufika na kupumzika katika nyumba ya rafiki yake.

Siku moja mwanamke huyu mwema alimwambia mumewe, "Naamini kwamba mchungaji Elisha anampenda Mungu sana. Nafurahi kwa sababu anataka kushiriki Neno la Mungu na watu wengine. Je, tungefanya nini ili tumsaidie?"

"Tunaweza kumjengea chumba. Pia, tutamwekea chumbani humo kitanda, kiti na meza. Ajapo tena atakuwa na chumba chake mwenyewe. Hata anaweza kupumzikia humo."

Mwanamke huyo na mumewe walifurahi sana. Walikuwa wamemtengenezea Elisha mahali pa kukaa.

Elisha naye, alifurahi sana. Alishukuru sana kwa ajili ya chumba hicho maalum alichojengewa na rafiki zake.

9. Waulize watoto waige mchezo wa kutembelewa na wageni. Chagua watoto watano. Wawili waweza kuwa nyumbani kwao; na wale watatu wawe wageni wao. Waambie watoto kuwakaribisha na kusalimia wageni wao vizuri. Wampatie kila mgeni kiti. Pengine "mama" atawapikia chai. Baadaye tena, chagua watoto wengine watano nao pia wawakaribishe wageni wao.
10. Wimbo: "Marafiki"
11. Kifungu cha Biblia: "Bwana Yu Mwema" (Zaburi 34:8). Rudia kifungu hiki pamoja na watoto.
12. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
13. Waonyeshe picha Namba 40. Ongea kuhusu Elisha na chumba hicho.
14. Omba ukimshukuru Mungu kwa ajili ya marafiki wanaotusaidia.



Somo la 41

# BOAZI MKULIMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Marafiki hunisaidia kupata chakula.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Nitakusaidia" (Isaya 41:10).

Nyimbo:

"Jumapili Yenye Furaha"
"Najua Mungu Ananitunza"
"Nisaidie Kuwa Mwema"

Tumia picha Namba 41.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Ruthu 2

Ruthu na Naomi walikuwa wajane. Walihamia Bethlehemu wakati wa mavuno. Kwa hivyo, hawakuwa na cho chote cha kuvuna. Waliwaona wafanya kazi wa Bethlehemu wakikata masazo ya nafaka na kuyafunga pamoja. Kulikuwa na desturi kwamba wakulima walitakiwa kuacha baadhi ya mavuno shambani ili walio maskini wapate kuyaokota. Hivi ndivyo Ruthu alivyopata chakula walichohitaji. Boazi, ambaye ni mwenye shamba, alikuwa rafiki aliyemsaidia Ruthu.

Siku hizi, marafiki husaidiana katika kazi ya shambani. Husaidia kulima na kupanda mbegu. Pia, husaidiana kuvuna mavuno. Hii ni sehemu ya mpango wa Mungu.

Naomi, mumewe na wanawe wawili walikuwa wameondoka Bethlehemu na kwenda kutafuta chakula kwa ajili ya njaa. Waliishi kwa miaka mingi sana katika nchi ya Moabu. Watoto wake walioa wasichana wa taifa la Moabu. Mmoja wao aliitwa Ruthu. Baada ya miaka michache wanawe Naomi pamoja na mumewe walikufa.

Ruthu aliamua kurudi Bethlehemu pamoja na Naomi. Alimsaidia mkwewe kwa kukusanya nafaka katika shamba la Boazi.

Soma Kitabu cha Ruthu 3 na 4. Ruthu aliolewa na Boazi, nao wakapata mtoto wa kiume. Walimwita Obedi. Naye Obedi alipata mtoto aitwaye Yese. Mtoto wa Yese naye aliitwa Daudi, ambaye alifanywa mfalme wa Israeli. Soma Luka 2:4. Yusufu alikuwa mmojawapo wa uzao wa Ruthu na Daudi.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto. Utapaswa kuinama ili watoto wakuone unapoongea nao.
2. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
3. Mwambie mtoto mmoja kuchukua chombo cha sadaka. Wengine watatakiwa kutembea hadi alipo wakiimba wimbo usemao, "Jumapili Yenye Furaha".
4. Ita kila jina na uweke alama katika kitabu cha rekodi.
5. Mchezo: Sema: "Kichwa, mabega, magoti, vidole." Shika mikono yako kwa sehemu ya mwili unayotaja. Waambie watoto nao wafanye hivyo. Rudia mchezo huu mara tatu. Baadaye sema, "sote



6. Nyimbo: "Msifuni Bwana", na "Usiku Walipoketi."
7. Uliza, "Kwa nini sisi husherehekea siku kuu ya kuzaliwa kwa Yesu?" Wape muda wa kufikiria na kujibu. Kama hawawezi kujibu, sema, "Mungu alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe," Wasomee kifungu hicho. Sema, "Nimeweka alama katika Biblia. Alama hiyo ipo katika mahali ambapo pana hadithi ya wachungaji waliomwona Yesu." Mwulize mtoto mmoja kufungua Biblia yako mahali ambapo umeweka alama hiyo.
8. **Acha Biblia Yako ikiwa Imefunguliwa katika Luka 2** na usimulie hadithi ya:

**WACHUNGAJI NA MALAIKA**

Ulikuwa usiku mtulivu. Nyota zilikuwa zikiangaza angani. Kondoo nao walikuwa wamejikufanya na kulala pamoja. Wachungaji nao walikua wamekaa katika mviringo, huku wakiota moto. Wakawa wanaongea kwa sauti za chini sana. Usiku huo ulikuwa mtulivu na wenye giza kuu.

Mwangaza mkuu uliwangaria kwa ghafula wachungaji hao. Walishangaa sana, na wakaingiwa na hofu kuu. Mwangaza huo ulikuwa mwingi sana hata hawakuweza kuangalia juu. Wakafunika nyuso zao.

Malaika aliwaambia, "Msiogope, kwa maana mimi nawaletea habari njema. Habari hii itawafurahisha sana. Na watu wote wataisikia habari hii."

"Yesu amezaliwa katika Bethlehemu. Yeye ndiye atakayekuwa Mwokozi wa ulimwengu. Mtampata akiwa amelala katika hori ya kulia ng'ombe."

Mara walitokezea wingi wa jeshi la malaika juu mbinguni. Wakaimba wimbo wa kumsifu Mungu. Waliimba hivi: "Atukuzwe Mungu juu mbinguni. Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

Wachungaji hao waliangaliana. Hatimaye mmoja wao akasema, "Haya na twendeni mpaka Bethlehemu. Tukamwone mtoto huyo tuliyeambiwa na malaika."

Wachungaji hao waliuzima moto wao. Wakachukua fimbo zao, na wakaenda kwa haraka hadi mjini. Pengine walipokuwa wakienda walizungumza na kuulizana maswali.

"Je, kweli twampata mtoto huyu?"

"Hebu fikiri tu. Malaika ndio waliotuletea habari hii njema."

Walipofikia mahali ambapo Yusufu na Mariamu walikuwa wanaishi, wakamwona mtoto Yesu. Alikuwa bado amelala katika hori ya kulia ng'ombe jinsi malaika alivyo waambia.

Wachungaji hao walimsifu Mungu kwa kutuma Yesu hapa duniani. Walimwambia kila mtu waliyemwona habari hii njema.

9. Sema, "Nataka kumshukuru Mungu kwa kumtuma mwanawe, Yesu. Je, nanyi pia mngependa kumshukuru Mungu?" Mruhusu ye yote anayetaka kuomba, aombe.
10. Mchezo: Waambie watoto kuiga mchezo wa kuzaliwa kwa Yesu. Utachagua baadhi ya watoto kuwa: malaika (aliyeongea na Mariamu), Mariamu, Yusufu, mwenye nyumba ya wageni, malaika mwengine, wachungaji, jeshi la malaika (usiwashirikishe mamajusi kwa sababu hao watakuwepo katika juma lijalo).
11. Wimbo: "Usiku Walipoketi"
12. Waonyeshe picha namba 51. Uliza, "Malaika aliwaambia wachungaji nini?"
13. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"



Somo la 51

# WACHUNGAJI NA MALAIKA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Malaika walisherehekea kwa nyimbo siku ya kuzaliwa kwa Yesu.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo" (Zaburi 69:30).

Nyimbo:
"Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"
"Usiku Walipoketi"
"Jumapili Yenye Furaha"
"Msifuni Bwana"

Tumia picha Namba 51.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 2:8-20

Wachungaji walikuwa wakilinda kundi la kondoo wao kwa zamu usiku. Malaika wa Bwana aliwaambia habari za kuzaliwa kwa Mwokozi. Baadaye malaika wengine waliimba nyimbo za kusifu kuzaliwa kwa Yesu.

Kwanza kabisa, wachungaji hao waliambiwa habari za kuzaliwa kwa Kristo. Mungu alijua kwamba wangeamini yale yote waliyoambiwa na malaika.

Waliogopa sana, walipo tokezewa na malaika. Soma yale waliyoambiwa na malaika katika kifungu cha 10. Malaika alikuwa na habari njema. Akawaambia, "Kristo, aliye Mwokozi, amezaliwa."

Mara wakaja wingi wa jeshi la malaika na kuimba nyimbo za kumsifu Mungu. Waliimba hizi, "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia", (Luka 2:14).

Wachungaji hao walienda kwa haraka sana hadi Bethlehemu. Walimkuta Mariamu, Yusufu na Mtoto Yesu akiwa amelala horini. Walimwambia kila mtu waliyekutana naye habari za ujumbe wa malaika.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Imbeni wimbo wa, "Jumapili Yenye Furaha" watoto waendeleapo kufika.
2. Sema, "Sisi humsifu Yesu kwa kuimba. Je, tunawezaje tena kumtukuza na kushiriki upendo wetu naye? Kwa kumtolea sadaka." Waambie watoto kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.
3. Mshukuru Mungu kwa sadaka hizo.
4. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe".
5. Soma Zaburi 69:30. "Nitalisifu jina la Mungu kwa wimbo." Rudia kifungu hiki pamoja na watoto. Uliza, "Kifungu hiki kinasema tumshukuruje Mungu?"



tupige makofi pamoja." Anzisha na mwendelee kwa muda.

6. Njoo na baadhi ya chakula cha kuwaonyesha watoto. Waweza kuleta ndizi, nyanya, mahindi au maharagwe. (Njoo na chakula ulichonacho kwako). Eleza jinsi vyakula hukua. Je, ni nani apandaye mbegu? Ni nani akusanyaye mavuno?

   Waonyeshe mahindi. Halafu sema, "Mwanamke mmoja katika Biblia alikusanya nafaka ili apate chakula. Mahindi ni aina ya nafaka. Mungu aliumba aina mbali mbali ya nafaka kama chakula cha watu - mahindi, mtama, shayiri, ngano na kadhalika.
7. **Fungua Biblia Yako katika Ruthu 2** na usimulie hadithi ya:

**BOAZI MKULIMA**

"Naomi, hatuna chakula. Nitaenda shambani na nikusanye nafaka," Ruthu akamwambia.

Muda si muda, Ruthu alilifikia shamba ambalo watu walikuwa wakifanya kazi.

"Je, naweza kuokota nafaka mnazoangusha?" akawauliza.

"Ndiyo, Boazi hawezi kukasirika iwapo utaokota." Watu hao wakamjibu.

Ruthu alikusanya nafaka nyingi sana. Baadaye Boazi, mkulima, alifika shambani. Alimwona Ruthu akiokota nafaka zilizoachwa.

"Je, mwanamke huyu ni nani?" akawauliza.

"Anaitwa Ruthu. Anatoka katika nchi ya Moabu. Naye anaishi na Naomi," wakamjibu.

Boazi mkulima, aliongea na Ruthu. "Waweza kuendelea kukusanya nafaka shambani mwangu. Usiende katika shamba lingine lolote. Pia, waweza kuuliza maji ya kunywa usikiapo kiu."

Ruthu akamwambia, "Asante sana. Mbona u mwema jinsi hiyo kwangu? Mimi ni mgeni tu katika nchi yenu."

"Nimesikia jinsi ulivyo mwema kwa Naomi. Nami nataka kuwasaidia," Boazi akamjibu.


Ruthu alifanya kazi hadi jioni sana. Alikusanya nafaka nyingi sana.

"Ruthu, umeokota wapi nafaka hii yote?" Naomi akamwuliza.

"Nilienda katika shamba la Boazi," Ruthu akamjibu. "Aliniambia kwamba naweza kurudi kila siku yote ili niweze kukusanya tena nafaka."

Naomi na Ruthu walimshukuru Mungu sana kwa ajili ya Boazi, rafiki yao. Walishukuru kwa kupata rafiki wa kuwasaidia.

8. Uliza, "Je, Ruthu alifanya nini kwa kumsaidia Naomi? Je, wewe humsaidia mama yako? Boazi alimsaidiaje Ruthu? Mungu anatutaka tuwasaidie wengine."
9. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema"
10. Wasaidie watoto ili wajifunze kifungu cha kukumbuka, "Nitakusaidia" (Isaya 41:10).
11. Waonyeshe picha namba 41 na ueleze kuhusu Ruthu na Boazi.
12. Wimbo: "Najua Mungu Ananitunza"
13. Mshukuru Mungu kwa ajili ya chakula atupacho.



Somo la 42

# MARAFIKI WANNE WEMA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Marafiki hunisaidia niwapo mgonjwa.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Rafiki hupenda siku zote" (Mithali 17:17).

Nyimbo-

"Yesu Ni Rafiki Mwema"
"Nisaidie Kuwa Mwema"
"Marafiki"

Tumia picha Namba 42.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Marko 2:1-12

Watu wengi walimwendea Yesu ili awaponye. Mtu mmoja hakuweza kutembea, kwa hivyo rafiki zake waliamua kumbeba hadi kwa Yesu. Wasaidie watoto kuelewa kwamba wao pia wanaweza kumsaidia rafiki yao akiwa mgonjwa.

Yesu alikuwa Kapernoumu kwa siku nyingi. Alifanya miujiza mingi sana akiwa huko. Alimponya mtumishi wa akida mmoja alipokuwa Kapernaumu (Mathayo 8:5-13), na pia mtoto wa diwani (Yohana 4:46-54). Pia, ilikuwa huko Kapernaumu ambapo mwujiza wa kuwalisha watu elfu tano ulifanyika.

Yesu alirudi tena Kapernaumu. Watu wengi walitaka kumwona. Kwa hivyo umati mkubwa wa watu ulikusanyika katika nyumba alimokuwa.

Yule kilema aliamini kwamba Yesu angemponya. Hata rafiki zake nao waliamini kuwa Yesu angemsaidia. Walimbeba hadi kwa Yesu ili amwone.

Soma tena kifungu cha 5. Kwanza kabisa, Yesu alimsamehe mtu huyo dhambi zake. Kwanza aliona ndani ya moyo wake. Hatimaye alimponya miguu yake. Halafu akamwambia, "Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi. Nakuambia, ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako."

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Uwe na kioo mkononi unapomsalimia kila mtoto. Sema, "Ninafuraha kwa sababu ______ amefika leo. Nikutazamapo, nakuona kama mtu maalum sana. Hebu angalia katika kioo hiki na unieleze yule unayemwona." Mwite kila mtoto kwa jina lake.
2. Wimbo: "Marafiki"
3. Mwambie kila mtoto afike mbele na kutoa sadaka yake.
4. Omba ukimshukuru Mungu kwa ajili ya sadaka.



7. Zungumza kuhusu zizi hilo. Uliza, "Ni nani waishio katika zizi?" (Ng'ombe, punda, mbuzi na wanyama wengine). "Je, ni nini mnachofikiria huwekwa ndani?" (majani, nyasi na pengine maji). Sema, "Miaka mingi iliyopita jambo fulani lilifanyika katika zizi la ng'ombe. Sikilizeni hadithi hii.
8. **Fungua Biblia Yako katika Luka 2** na usimulie hadithi ya:

**KUZALIWA KWA YESU**

"Mfalme amesema kwamba kila mtu aende kijijini mwake. Yampasa kila mmoja kwenda na kuandika jina lake katika kitabu. Kwa hivyo tutatakiwa kwenda Bethlehemu," Yusufu akamwambia.

Mariamu alijua kwamba ingekuwa safari ndefu sana. Alijua pia kwamba Mungu angewatunza. Mariamu kapanda juu ya punda. Safari yao ilianza. Yusufu alimwongoza punda barabarani.

Yusufu alijua kwamba Mariamu amechoka. Kwa hivyo walipumzika mara kwa mara. Walikutana na watu wengi sana huko barabarani. Kila mmoja alikuwa akirudi kijijini kwao kufuatia agizo la mfalme.

"Yusufu, je, tungali mbali kufika?" Mariamu akamwuliza.

Waliufikia mlima, na mbele yake, Yusufu aliweza kuona kijiji kile vizuri sana. "Tazama, Bethlehemu ndipo pale. Muda si muda tutafika mahali hapo."

Mariamu alifurahi sana wakati punda wao alipotembea katika kijiji hicho. Yusufu naye alienda hadi katika nyumba ya wageni.

"Bwana, tunahitaji mahali pa kulala usiku wa leo. Tumesafiri safari ndefu sana na tumechoka sana," Yusufu akamwambia.


"Samahani sana, hakuna nafasi ye yote. Watu wengi wamefika mjini, kwa hivyo hakuna nafasi katika chumba cho chote," mtu huyo akamjibu.

Mtu huyo alimwona Mariamu akiwa mchovu sana. Akamwambia, "Unaweza kwenda kulala katika zizi la ng'ombe. Nitakutafutia majani mazuri ya kulalia. Samahani sana kwa sababu hapo ndipo pana nafasi tu."

Yusufu alimwangalia Mariamu. Mariamu akamwambia, "Ndiyo, Yusufu, nilazima twende kupumzika."

Usiku huo huo, mtoto Yesu alizaliwa. Mariamu alimfunga katika nguo nyororo na yenye joto. Akamlaza katika hori ya kulia ng'ombe.

9. Sema, "Nataka kumshukuru Mungu kwa kumtuma Yesu." Uliza, "Je, mmoja wenu angependa kuomba?"
10. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"
11. Sema, "Sisi Wakristo husherehekea siku kuu ya kuzaliwa kwa Yesu kwa sababu 'Mungu alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe' ". Waambie watoto kusema kifungu hicho. Baadaye tazameni katika 1 Yohana 4:10. Onyesha watoto kifungu hicho. Sasa waambie tena kukisema pamoja nawe. "Mungu... alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe," (1 Yohana 4:10).
12. Waonyeshe picha namba 50. Ongea kuhusu Mariamu na mtoto Yesu. Waeleze kwamba zizi huwa na ukuta, pamoja na paa. Hori ya kulia ng'ombe, ni sehemu ambayo huwekwa nyasi, yaani chakula cha ng'ombe. Hori hili huwa kavu na safi sana.
13. Ongea kuhusu wanyama ambao walikuwemo katika zizi hilo. Waache watoto waseme majina yao. Uliza, "Je, mnafikiri ng'ombe walimsaidiaje Yesu?" (Walimpatia Yesu hori ambalo alililalia). "Je, punda naye alimfanyiaje?" (alimbeba Mariamu hadi Bethlehemu). "Nao kondoo walisaidiaje?" (Walitoa manyoya yao ambayo yalitumiwa kama blanketi).
14. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe."



Somo la 50

# KUZALIWA KWA YESU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Yesu, Mwana wa Mungu, alizaliwa.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu... alitupenda sisi, akamtuma Mwanawe", (1 Yohana 4:10).

Nyimbo:
"Yesu Anawapenda Watoto Wote"
"Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"

Tumia picha Namba 50.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 2:1-7

Mariamu na Yusufu walisafiri hadi Bethlehemu kulipa kodi yao na pia kujiandikisha. Walilala katika zizi la ng'ombe kwa sababu hakukuwa na nafasi katika chumba cho chote. Mariamu alimzaa mtoto Yesu, walipokuwa wamelala katika zizi hilo. Alijua kwamba mtoto huyo ndiye yule aliyeahidiwa na Mungu.


Mariamu na Yusufu walisafiri mwendo wa kilomita 115. Walitakiwa kwenda Bethlehemu kwa sababu huko ndiko alikozaliwa Yusufu. Wote walitakiwa kwenda kujiandikisha. Bethlehemu ni mojawapo ya miji ya zamani sana iliyoko Israeli. Nabii Mika alikuwa ametabiri kwamba Masihi angezaliwa katika mji huu.

Je, mnakumbuka somo letu lililopita kuhusu Ruthu na Boaz? Rudia tena somo la 41. Boazi alimzaa mtoto aitwaye Obedi. Obedi naye alimzaa Yese. Naye mtoto wa Yese, yaani Daudi, alikuwa mwenye ukoo wa Yusufu. Mpango wa Mungu wa kuzaliwa kwa Yesu ulikuwepo miaka mingi sana kabla ya Yusufu na Mariamu kwenda kuishi Bethlehemu.

Watu wa Bethlehemu hawakuwa na habari kwamba Masihi alikuwa amezaliwa. Hata Yusufu na Mariamu hawakuelewa vizuri jambo hili. Lakini walijua kwamba wao wamo katika mpango huo wa Mungu.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto. Sema, "Leo nimefurahi sana. Nimefurahi kumwona tena ______ siku ya leo."
2. Sadaka: Sema, "Njia moja ambayo twaweza kushiriki furaha yetu ni kwa kumtolea Mungu sadaka zetu."
3. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
4. Rekodi: Mwambie kila mtoto asimame unapoita jina lake.
5. Wimbo: "Yesu Anawapenda Watoto Wote"
6. Kazi: Tengeneza zizi la ng'ombe. Tumia vijiti, udongo na uezeke na nyasi zilizokauka. Linaweza kuwa kama mchoro huu. (Tazama mchoro huo.) Waambie watoto wakusaidie kujenga.





5. Wimbo: "Yesu ni Rafiki Mwema"
6. Sema, "Mimi hufurahi sana ninaposikia kwamba Yesu ni rafiki wetu mwema. Yesu aliwasaidia watu kila mara. Mwakumbuka kifungu cha Biblia kisemacho, 'Yesu...akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema' (Matendo 10:38). Je, mnaweza kufikiria kifungu kimoja kituambiacho tusaidiane?" Tazama 2 Wakorintho 1:24 (K.J.V.): "Tu wasaidizi".
7. Wimbo: "Marafiki"
8. Sema, "Ni vizuri kuwa na marafiki. Katika Mithali 17:17, Biblia inasema kwamba, "Rafiki hupenda siku zote." Rudieni kifungu hiki mara nyingi.
9. **Fungua Biblia Yako katika Marko 2** na usimulie hadithi ya:

**MARAFIKI WANNE WEMA**

"Watu wanne walikuwa wakijadiliana. "Yesu yuko mjini. Anawahubiria watu. Natamani sana rafiki yetu mgonjwa amwone. Naamini kwamba Yesu atamponya."

Walienda hadi kwa nyumba ya rafiki yao. Alikuwa amelala kitandani. Hakuweza kutembea. Kwani miguu yake haikufanya kazi.

"Rafiki, Yesu yuko mjini. Je, utaenda kumwona?" wakamwuliza.

"Ndiyo, natamani sana kumwona. Lakini naendaje? akawauliza.

"Tutakubeba ukiwa juu ya godoro lako", wakamwambia. Walimbeba mtu huyo kwa uangalifu akiwa juu ya godoro lake.

Waliona watu wengi sana walipofika karibu na nyumba ile Yesu alikuwemo. Yule mgonjwa akawaambia, "Nadhani sitaweza kumwona Yesu, kwa sababu kuna watu wengi sana."


Rafiki hao wanne walipanda hadi juu ya paa la nyumba. Wakamweka mgonjwa huyo chini. Wakaanza kutoboa shimo katika paa hilo. Mwishowe kulikuwa na shimo kubwa sana. Hata waliweza kumwona Yesu vizuri sana.

Walimtelemsha rafiki yao chini wakitumia kamba. Yesu alipomwona mtu huyo akasema, "Jitwike godoro lako na uende."

Mgonjwa alisimama mara moja. Miguu yake ikaanza kufanya kazi. Hata aliweza kutembea.

Rafiki zake walifurahi sana kwa sababu waliweza kumsaidia.

10. Uliza, "Je, unajua mtu ye yote ambaye ni mgojwa?" Kama watoto wanamjua mtu ye yote, basi waelezee njia ambazo wanaweza kumsaidia nazo. (Wanaweza kuwa kimya, wawatunze wale walio wadogo, wampelekee maua, au wamsaidie kuchunga mbuzi na kadhalika).
11. Fanyeni mchezo wa kushiriki. Waambie watoto wakae katika mviringo na waweke mikono katika mapaja yao. Jifanye kama unamwekea kila mmoja jiwe dogo mkononi mwake. Mpe mtoto mmoja jiwe hilo, na wengine wabahatishe ni yupi aliyenalo. Baadaye mtoto huyo naye ataweka jiwe hilo, na wengine wabahatishe ni yupi aliyenalo. Baadaye mtotc huyo naye ataweka jiwe hilo katik mkono wa mwenzake. Endeleer hivyo kwa muda.
12. Wimbo: "Nisaidie Kuwa Mwema
13. Waonyeshe picha namba 42. Hasa waonyeshe wale marafiki walioko juu ya paa la nyumba.



Somo la 43

# RAFIKI WA KIPOFU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Yesu husaidia wakati hatuna wa kutusaidia.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Yesu... akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema" (Matendo 10:38).

Nyimbo:

"Jumapili Yenye Furaha"
"Msifuni Bwana"
"Yesu Awasaidia Wagonjwa"

Tumia picha Namba 43.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Yohana 9

Yesu alimponya kipofu ili kudhihirisha uwezo wa Mungu. Hakukuwa na mtu ye yote ambaye aliweza kumponya kipofu huyo. Alimsifu na kumtukuza Yesu na kumkubali kama Mwana wa Mungu. Wasaidie watoto kujua kwamba Yesu angali anatusaidia hata leo.

Yesu na wanafunzi wake walienda Yerusalemu kwa ibada. Alimwona mtu ambaye alihitaji msaada. Mtu huyu alikuwa kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake waliwaza ni nani aliyesababisha upofu wake. Yesu alijua mawazo yao, na akawaambia kwamba upofu wake hukutokana na dhambi zake wala za wazazi wake.

Mtu huyu alipoponywa alimtukuza Yesu na kumshukuru kwa kumponya na kuweza kuona. Mafarisayo walijaribu kumshawishi mtu huyu akubali kwamba alikuwa akiona mbeleni, lakini mtu huyo aliwaambia tu ukweli. Yesu alikuwa amemponya.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto anapofika. Uliza, "Je, mliona nini njiani mlipokuwa mnakuja kwa Shule ya Jumapili?" Ngoja jibu la kila mmoja.
2. Wimbo: "Msifuni Bwana."
3. Chagua watoto wawili wa kuchukua chombo cha sadaka hadi kwa wenzao.
4. Omba, ukimshukuru Mungu kwa ajili ya baraka zake.
5. Ita kila jina na uweke alama kwa majina ya waliohudhuria.
6. Mchezo: Waambie watoto wafumbe macho yao. Uliza, "Je, mnaona nini? Waambie wafumbue macho yao, sasa chagua mtoto mmoja. Mwulize hivi, "Je, kama hungeweza kuona, ungejuaje watoto wengine?" Mfunge huyo mtoto kwa kitambaa usoni. Sema, "Tumechagua rafiki. Tunataka umtambue. Sikiliza tu sauti yake." Mtoto mwingine atasema, "Niko hapa". Mwulize yule mtoto aliye-



furaha?" Wape muda wafikirie na wajibu.

9. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
10. Uliza, "Je, nyinyi hufurahi msikiapo jambo zuri ambalo linasemekana litatokea? Ni najua hadithi ya Biblia kuhusu msichana mmoja aliyepata habari kwamba jambo jema lingetokea."
11. **Fungua Biblia Yako katika Luka 1** na usimulie hadithi ya:

### MALAIKA AMTEMBELEA MARIAMU

Siku moja, Mariamu alikuwa akifanya kazi nyumbani kwao. Akasikia sauti ikiongea naye.

"Umebarikiwa. Mungu yu pamoja nawe," Malaika akamwambia.

Mariamu alifadhaika sana aliposikia maneno ya malaika. Hakujua angeendelea kumwambia nini.

"Mariamu, usiogope. Nina habari njema ya kukuambia. Utachukua mimba na kumzaa mtoto. Utamwita Yesu. Huyo atakuwa mkuu. Naye atakuwa Mwana wa Mungu".

Malaika aliondoka, alipomaliza kuongea na Mariamu. Naye Mariamu alifurahi sana alipofikiria zaidi kuhusu ujumbe huu. Aliamua kwenda na kumtembelea Elizabeti, binamu yake. Alitaka amwambie Elizabeti habari hii njema.

Mariamu alimsalimia Elizabeti alipofika nyumbani kwake. Naye Elizabeti alipomsikia Mariamu akiongea, alijua kwamba ana habari njema. "Mariamu, umebarikiwa sana na Mungu," akamwambia.

Mariamu na Elisabeti, waliongea kwa muda mrefu sana pamoja. "Namshukuru Mungu sana," Mariamu akamwambia. "Roho yangu imemfurahia Mungu. Kwani yeye atanitumia. Vizazi vyote vitaniita mbarikiwa. Mungu ni mwenye uwezo. Naye amenitendea makuu."

"Jina lake ni takatifu. Naye ni mwenye rehema, pia na nguvu. Atawatawanya walio na kiburi. Lakini atawakweza walio wanyenyekevu."

"Mungu alikuwa ameahidi kuwaokoa watu wake. Naye angewaokoa kupita kwa Yesu."

Mariamu alikaa kwa Elizabeti kwa muda wa miezi mitatu. Baadaye, siku moja akasema, "Nimefurahi sana kuishi pamoja nawe. Lakini sasa nami nataka nirudi nyumbani kwangu."

12. Waonyeshe picha namba 49. Je, habari njema ya Mariamu ilikuaje? Waambie watoto habari ya malaika na Mariamu.
13. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"
14. Maombi: "Asante sana, Mungu, kwa kutupa wakati wa furaha. Asante pia kwa wakati tupatapo habari njema. Asante kwa kumpatia Mariamu habari njema ya kwamba Yesu atazaliwa."
15. Mchezo: Sema, "Kila mmoja asimame wima. Sasa, shikeni vidole vyenu vya miguu. Nifuateni ninapotembea darasani. Waambie tena wafanye kitendo kingine unachotoa.
16. Kazi ya kufanya: Kaeni katika mviringo. Sema, "Ninazo habari njema. Nitamwambia ________." (Sema jina la mtoto aliyekaa karibu nawe). Naye atamwambia yule aliyekaa karibu naye. Endeleeni na kupasha habari hiyo hadi kila mmoja atakapo mwambia mwenzake aliyekaa karibu naye. Ujumbe wenyewe ni kwamba: "Mungu anakupenda."
17. Wimbo: "Yesu Ananipenda"



Somo la 49

# MALAIKA WAMTEMBELEA MARIAMU

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mariamu aliambiwa habari njema.

**Kifungu cha Kukumbuka:** " 'Nitamwimbia Bwana' " (Kutoka 15:1).

Nyimbo:

"Mungu Alitupenda na
"Akamtuma Mwanawe"
"Yesu Anipenda"
"Napenda Kanisa"
"Leo Tunafuraha"

Tumia picha Namba 49.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Luka 1:26-56

Malaika alimpelekea Mariamu ujumbe kutoka kwa Mungu. Soma vifungu hivi, 46-55. Mariamu aliimba wimbo huu wa kumtukuza Mungu. Wafundishe watoto kwamba Mariamu alifurahi sana aliposikia ujumbe huo wa malaika.

Mariamu alikuwa bado msichana sana. Hakuwa ameolewa, lakini alikuwa ameposwa na Yusufu. Ujumbe huu wa Mungu ulisema kwamba angemzaa Mwana wa Mungu. Na aliambiwa kwamba jina lake litakuwa Yesu.

Mariamu alikuwa na moyo wa kufanya yote yale ambayo Mungu angemwambia. Alimwambia malaika huyo kwamba yeye atamtii Mungu tu.

Lakini Mariamu alikuwa na swali la kuuliza. Kifungu cha 34 kinasema kwamba, "Litakuaje neno hili, maana sijui mume?" Malaika alimjibu kwamba, Roho Mtakatifu ndiye angetekeleza hayo yote.

Mariamu alifurahi sana. Alishukuru kwa sababu Mungu alikuwa amemchagua kwa kazi maalum.

Wayahudi walikuwa wakingojea Masihi. Mariamu aliamini kwamba Mungu alikuwa sasa amemtuma Masihi. Hata hivyo, alimshukuru Mungu sana kwa kumchagua.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Fika mapema. Mkaribishe kila mtoto afikapo.
2. Wimbo: "Napenda Kanisa"
3. Waambie watoto wawili kupitisha chombo cha sadaka kati yao ili wote waweze kuweka sadaka zao.
4. Maombi: Omba, "Bwana, nakutolea sadaka hii kwa sababu wewe ndiye unipaye vyote nilivyo-navyo."
5. Ita kila jina na uweke alama katika kitabu chako cha rekodi.
6. Wimbo: "Alitupenda na Akamtuma Mwanawe"
7. Weka alama katika Biblia yako, katika Kutoka 15:1. Mwulize mtoto mmoja kufungua Biblia hiyo mahali ambapo kuna alama. Wasomee watoto kifungu hicho, "Nitamwimbia Bwana". Waambie wajifunze kifungu hicho hadi watakapokijua vizuri.
8. Uliza, "Je, leo mnafuraha? Ni nini kilichowafanya mwe wenye



fungwa macho yake kubahatisha jina la yule aliyeongea. Kama hawezi kumtambua, basi mpeleke hadi kwa mtoto yule na umwambie amguse. Sasa mwulize kama anaweza kumtambua. Mwishowe mfungue kitambaa kutoka machoni mwake.

7. Ongea kuhusu kutokuona kulivyo. Sema, "Nashukuru kwa sababu naweza kuona, na weweje?"
8. Omba, "Asante Mungu, kwa sababu tunaweza kuona vitu vyote ulivyoumba."
9. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
10. **Fungua Biblia Yako Katika Yohana 9** na usimulie hadithi ya:

**RAFIKI WA KIPOFU**

Mtu mmoja alikaa kando ya barabara. Akasikia watu wakitembea na kupita mahali hapo. Alisikia sauti nyingi tofauti lakini hakuona cho chote. Alikuwa kipofu.

Alikuwa kipofu tangu kuzaliwa. Hakuweza kuona kamwe. Ila kila siku alikaa tu kando ya barabara. Alikuwa akiomba pesa za kujinunulia chakula.

Siku moja Yesu alipita mahali hapo. Akamwona mtu huyo. Hatimaye alitengeneza tope kwa mate yake na kuupaka machoni mwa kipofu huyo.

Baadaye Yesu akamwambia, "Nenda kanawe katika birika la Siloamu."

Kipofu huyu alifanya jinsi alivyoambiwa na Yesu. Aliendа katika kiziwa hicho na akanawa uso wake.

Alipoosha tope hilo kutoka usoni, aliweza kuona vizuri. Akaangalia pale alipokuwa amesimama. Akaona mbingu ya rangi ya samawati (buluu). Akaona tena wanaume na wanawake wakitembea.

Alifurahi sana akapaza sauti akisema, "Naweza kuona."

Jirani zake walimwangalia. Hata wakaulizana, "Je, huyu ndiye yule kipofu?"

Mtu huyo aliwajibu, "Ndiyo, ni mimi. Mtu aitwaye Yesu alitengeneza tope, halafu akanipaka machoni mwangu. Mwishowe akaniambia niende kunawa uso wangu. Ndiyo maana sasa naweza kuona."

"Haiwezekani hivyo. Umekuwa kipofu siku zote," wakamjibu.

"Naweza kuona," akawaambia tena. "Rafiki yangu, Yesu, amenisaidia."

11. Uliza, "Je, Yesu alifanya nini alipomsaidia kipofu yule kuona?" Ngojea watoto waseme yale aliyo-fanya Yesu. Alitema mate, akatengeneza tope, akapaka tope hilo machoni mwa kipofu yule.
12. Waonyeshe picha namba 43. Eleza jinsi kijana yule anavyomsaidia huyo kipofu.
13. Kifungu cha Biblia: Twasoma katika Biblia kwamba: "Yesu... akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema" (Matendo 10:38). Waambie watoto warudie kifungu hiki. Sema, "Uponyaji wa kipofu yule ni baadhi ya kazi njema ambayo Yesu alifanya."
14. Wimbo: "Yesu Awasaidia Wagonjwa"
15. Mwambie kila mtoto kuchagua rafiki. Mmoja kati yao afumbe macho yake. Mwenzake amshike mkono naye akimwongoza darasani. Baadaye mwenzake naye afumbe macho ili naye pia aongozwe kutembea darasani.
16. Maombi: Mshukuru Mungu kwa sababu tunaweza kuona, na kwa ajili ya mikono na miguu ambayo twatumia kuwasaidia wengine.



Somo la 44

# USIKU NA MCHANA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alipanga kuwepo na usiku na mchana.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu akaita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku" (Mwanzo 1:5).

Nyimbo:

"Dunia Ya Mungu"
"Napenda Kanisa"

Tumia picha Namba 44.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 1:1-5, 14, 8:22, 28:10-16, Zaburi 104:19-23

Vifungu hivi vyatueleza muumbo wa Mungu. Yeye ni Mungu aliye Mkuu. Alikuwa na mpango alipouumba ulimwengu. Aliumba·mchana kwa ajili ya kufanya kazi; na usiku kwa ajili ya kupumzika. Huu ni mpango wa Mungu.

Dunia ilikuwa giza tupu, ndipo Mungu akakata shauri kuumba nuru. Aliita nuru hiyo Mchana. Aliumba mchana katika siku ya kwanza ya muumbo wake. Na siku ya nne ndipo alipoumba jua.

Giza liliitwa usiku. Kwa hivyo, mwezi na nyota ziliumbwa ili kutoa mwangaza wakati wa usiku.

Soma Mwanzo 28:10-16. Yakobo alikuwa akisafiri, na kulipokuchwa alisimama ili apumzike. Akaweka kichwa chake juu ya jiwe. Alipokuwa akilala aliota ndoto. Mungu alimwekea Yakobo ahadi. Alimwambia kwamba atakuwa pamoja naye na atamtunza pia.

Yakobo alimshukuru Mungu kwa ahadi yake alipoamka.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Karibisha watoto. Shikaneni mikono wakati watoto wawili au watatu wafikapo, na mfanye mviringo. Imbeni, "Jumapili ni siku njema. Sisi huja kanisani. Jumapili ni siku ya furaha, ndiyo maana tunaimba."
2. Waambie watoto kwenda hadi mahali pa chombo cha sadaka wakiimba, "Napenda Kanisa," na kuweka sadaka zao humo.
3. Mwambie kila mtoto asimame unapoita jina lake. Weka alama katika kitabu cha rekodi.
4. Wimbo: "Kichwa, mabega, magoti, vidole" (Maneno ya wimbo na vitendo yameelezwa katika somo la 41.)
5. Uliza, "Je, nini hufanyika wakati jua linapokuchwa wakati wa jioni?" (Huwa na giza) "Je, na wakati wa usiku nyinyi.huona nini?" (Mwezi na Nyota) Sema, "Mungu alikuwa mwema alipoumba mwezi na nyota ili kutoa mwangaza wakati wa usiku. Je, wewe hupenda kufanya nini wakati wa usiku?" (Kusikiliza



Soma Mhubiri 3:11. "Kila kitu amekifanya kizuri." Rudia kifungu hiki pamoja na watoto.

10. **Fungua Biblia Yako katika Mwanzo 1** na usimulie hadithi ya:

**ULIMWENGU MZURI**

Mungu aliumba mbingu na nchi. Aliumba pia nuru na giza. Aliita nuru mchana na akaliita giza usiku.

Mungu aliumba nchi na maji. Akaifanya mimea na miti kukua. Aliumba mwezi, nyota na jua. Akawaumba wanyama watembeao. Aliwaumba samaki waogeleao baharini na ndege warukao angani. Alimwumba pia mwanadamu.

Mungu aliiumba milima mirefu sana. Akaumba na hata mabonde. Aliikuza miti mirefu na kijani kibichi mabondeni na akaifanya mito kupita humo.

Mungu aliumba najangwa yaliyokauka na yenye mchanga mweupe sana. Akalifanya jua litoe mwangaza na joto.

Mungu aliumba ndovu wakubwa wenye ngozi ngumu. Aliwaumba pia sungura wenye manyoya laini na nyororo. Aliumba hata swara wakimbiao haraka sana. Simba nao waliumbwa na manyoya mengi yafunikayo vichwa vyao. Aliwaumba hata chui wenye madoadoa ya kupendeza.


Aliyakuza maua mazuri ya kupendeza. Kuna maua mekundu na ya majano. Kunayo pia meupe na ya aina ya buluu.

Mungu aliipangia mvua kunyesha. Mvua huifanya miti na maua kukua.

Mungu aliwaumba watu ili waishi katika ulimwengu huu wake. Watu nao wanayo mikono ya miguu iwasaidiapo kutembea na kufanya kazi. Wanayo macho, hata wanaweza kuona. Wana sauti nzuri za kuimba. Wana hata mioyo ambayo imejua upendo.

Mungu aliumba kila kitu. Vitu hivi vyote vinatofautiana. Kila kimoja kina maumbile yake. Kweli, Mungu aliumba kila kitu kikawa kizuri.

11. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
12. Sema, "Mungu aliumba kila kitu na kikawa kizuri, lakini mwanadamu hajatunza ulimwengu huu jinsi Mungu alivyonuwia. Miti mingi inakatwa kila siku. Naye akataye hata hawezi kupanda mti mwingine mahali hapo palipokatwa. Sasa maana sehemu nyingi hazina miti ile iliyopandwa na Mungu. "Baadhi ya babu na nyanya zetu walilima katika hali isiyofaa na wakauacha udongo wenye rutuba kuchukuliwa na maji hadi mitoni. Hata kuna viwanda fulani ambavyo hutupa mabaki ya takataka zao baharini au mitoni. Hata sasa tumeshindwa kabisa kutunza vizuri ulimwengu huu mzuri ambao ni muumbo wa Mungu. Je, unaweza kufikiria jambo ambalo tukilifanya pamoja tutaongezea uzuri mwingi kwa ulimwengu huu?"
13. Pangeni na watoto ili waweze kupanda miti, kupanda maua au kusaidia kujenga matuta katika shamba. Tafuteni siku moja nzuri inayofaa na mfanye mradi huo. Fanyeni hivyo juma hili.
14. Waonyeshe picha namba 48. Waache watoto wataje vitu ambavyo wanaona ni vya kupendeza katika picha hiyo. Waambie wote waseme yaani wasichana kwa wavulana.
15. Omba, "Asante, Mungu, kwa kuumba ulimwengu ambao ni mzuri kwetu."
16. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"



Somo la 48

# ULIMWENGU MZURI

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alipanga na akaumba ulimwengu mzuri.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Kila kitu amekifanya kizuri" (Hubiri 3:11).

Nyimbo:

"Jumapili Yenye Furaha"
"Dunia Ya Mungu"
"Napenda Kanisa"

Tumia picha Namba 48.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 1 na 2; 9:12-16

Maandiko haya yanaeleza jinsi ulimwengu ulivyoumbwa. Yanaonyesha uwezo na hekima ya Mungu. Mungu alikuwa na mpango wa cho chote alichoumba. Hata mwenyewe alisema, "Tazama, ni chema sana."

Tangu mwanzo, Mungu aliumba nuru ili itenganishe mchana na usiku. Aliumba anga, nchi, maji ya bahari na aina yote ya mimea. Aliumba jua na mwezi. Akawaumba samaki wa baharini na ndege warukao angani. Aliwaumba wanyama wote waishio. Mwishowe, Mungu alimwumba mwanadamu. Hapo alitoa siku ya kupumzika.

Ukiangalia maumbile, utatambua kwamba Mungu ndiye mwumbaji wa vyote. Maua huwa ya kupendeza. Mawingu nayo hupendeza yaonekanapo angani.

Mungu alimpatia mwanadamu mamlaka ya kutunza muumbo wake mzuri hapa duniani. Sisi hukumbuka upendo wa Mungu kwa mwanadamu. Tuonapo muumbo wake.

Soma Mwanzo 9:12-16. Mungu alimpatia mwanadamu upindi wa mvua kama ishara. Alifanya ahadi ya kutomwangamiza mwanadamu kwa mafuriko kwa sababu anampenda sana.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Fika mapema ili uweze kumsalimia kila mtoto. Mpe kila mtoto ua au jani la mti afikapo. Sema, "Ninafurahi kwa sababu ________ amefika leo."
2. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
3. Imbeni, "Napenda Kanisa," Watoto watembeapo na kwenda kuweka sadaka zao katika chombo cha sadaka.
4. Maombi: Omba, "Asante sana, Mungu, kwa zawadi zako. Tunakutolea tena kwa sababu tunakupenda."
5. Ita jina la kila mtoto na umwulize ataje kitu kilichoumbwa na Mungu. Weka alama katika kitabu chako cha rekodi.
6. Kusanya yale maua uliyowapatia watoto. Yaweke katika chupa na uache darasani.
7. Eleza kuhusu maua hayo. Je, yana rangi gani? Je, yananukia? Ni nani aliyeyaumba? Sema, "Ndiyo, Mungu aliyaumba ili ulimwengu uonekane maridadi."
8. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
9. Sema, "Tunajua kwamba Mungu aliumba ulimwengu mzuri kwa sababu Biblia inatuambia hivyo."



hadithi, kuota moto, kula, kuwa pamoja na wazazi wangu, kulala).

6. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
7. Biblia inatuambia kwamba "Mungu akaita nuru mchana, na giza akaliita usiku" (Mwanzo 1:5). Rudia kifungu hiki hadi watoto watakapokielewa vizuri.
8. Sema, "Biblia inatwambia mambo mengi kuhusu Mungu. Je, mnafurahia Biblia?"
9. Wimbo: "Twaipenda Biblia"
10. **Fungua Biblia Yako Katika Mwanzo 28:10-16** na usimulie hadithi ya:

USIKU NA MCHANA

Mungu aliumba mbingu na nchi. Kwanza kabisa hapakuwa na nchi, wala cho chote. Kulikuwa tu giza tupu. Hakukuwa na nuru yo yote.

Mungu akasema, "Iwe Nuru."

Nuru ilitokea. Mungu aliona kwamba nuru inapendeza. Akaita wakati huu wa nuru mchana. Na akaita wakati wa giza usiku.

Mwishowe Mungu alitoa ahadi. Alisema kwamba jinsi nchi inavyodumu vivyo hivyo kutakuwepo mchana na usiku.

Yakobo alikuwa safarini. Naye alikuwa ametembea kwa muda mrefu sana. Ilipofika usiku, hakuwa na mahali pa kulala. Aliweka jiwe kubwa chini ya kichwa chake na akalala usingizi. (Onyesha picha namba 44).

Alipokuwa akilala aliota ndoto. Mungu alisema naye katika ndoto hiyo. Mungu alimwambia, "Nitakulinda. Tena niko pamoja nawe kila uendako."

Yakobo aliamka baada ya kuota ndoto hiyo. Akasema, "Kweli Bwana yupo mahali hapa. Naye atanilinda."

Yakobo alifurahi sana usiku huo wote. Alifurahi kwa sababu alipata muda wa kupumzika. Alifurahi pia, kwa sababu Mungu aliahidi kuwa pamoja naye na kumtunza.

Miaka mingi baadaye mtu mmoja aliandika wimbo kuhusu usiku:

"Mungu aliumba mwezi na majira.
Jua hujua wakati wa kuchwa.
Mungu aliumba giza.
Wanyama hutoka mwituni wakati wa usiku.
Watoto wa Simba hutafuta chakula.
Wakati wa mapambazuko, wao hutoroka,
Huenda kulala katika pango.
Mwanadamu naye huamka. Na kufanya kazi hadi jioni"

11. Je, huu si ni wimbo mzuri? Unapatikana katika kitabu cha Zaburi.
12. Mchezo: Sema, "Hebu tujifanye kuwa vifaranga wanao tafuta chakula. Mimi nitakuwa mama wenu. (Zunguka huko na huko ukiwaita watoto ili waweze "kudonoa" chakula). "Sasa usiku umeingia. Cluck, cluck, njooni vifaranga wangu", (watoto wanaweza kuchuchuma karibu na mwalimu na wajifanye kuwa vifaranga waliolala).

    "Sasa wawe watoto wanaocheza wakati wa mchana. (Watoto wanaweza kuimba na kucheza). Hatimaye imekuwa usiku. Ni lazima sasa walale." (Watoto wajifanye kuwa wamelala).
13. Maombi: "Niendapo kulala, najua kwamba Mungu atanilinda. Niamkapo asubuhi, humshukuru Mungu kwa ajili ya kunilinda usiku kucha".



Somo la 45

# MVUA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu hutupatia mvua.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu wetu, aletaye mvua" (Yeremia 5:24).

Nyimbo:
"Leo Tunafuraha"
"Dunia Ya Mungu"

Tumia picha Namba 45.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** 1 Wafalme 17:1, 18:1-2, 41-45; Isaya 55:10, Yoeli 2:23

Vifungu hivi vinatusaidia kufahamu kwamba Mungu ndiye anayeitawala mvua. Mungu aliumba dunia na vyote vijazavyo. Mungu aliipangia mvua kuinyeshea dunia. Mbegu nazo hukua na kutupa chakula.

Katika Wafalme wa Kwanza, twasoma kuhusu Eliya, nabii wa Mungu. Mungu alimtuma Eliya kumwonya Ahabu, mfalme wa Israeli. Mungu hangewapatia mvua kwa muda wa miaka mitatu. Watu hawakuwa na chakula wala maji. Ng'ombe walikuwa wakifa; na hapakuwa na mazao yo yote.

Mungu alisema tena na Eliya. Alimwambia kwamba ataleta mvua. Soma 1 Wafalme 18:41-45. Mvua ilianza kunyesha jinsi Mungu alivyosema. Hii ilionyesha uwezo wa Mungu.

Soma Isaya 55:10. Mungu hutuma mvua. Mvua huzifanya mbegu kutoa mazao. Wanyama nao hupata nyasi, chakula chao. Kila mmoja huwa na chakula.

Tunaambiwa katika Yoeli 2:23 kwamba, yatupasa kufurahi na kumshukuru Mungu kwa kutupa mvua. Hili ni somo ambalo watoto wataelewa kwa urahisi. Mungu hutuma mvua ili watu, mimea na wanyama wapate maji.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto. Sema, "Nimefurahi kwa sababu umefika leo. Hebu angalia kila mahali ili uone kitu ambacho Mungu ameumba." (Weka juu ya meza au kwenye mkeka vifaa mbali mbali vya muumbo kama nyasi, jiwe, mahindi, mdudu na kadhalika).
2. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
3. Waambie watoto watoe sadaka zao wafikako.
4. Ita kila jina na uweke alama kwa wale waliohudhuria.



5. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
6. Uliza, "Je, mlipokuwa mnakuja kanisani mliona nini njiani?" "Niliona kitu cheupe na kikubwa sana." "Je, kilikuwa nini?" (Wingu). Ngojea kila mtoto aseme kile alichoona njiani alipokuwa akija.
7. Kifungu cha Biblia: "Mungu huyameesha majani" (Zaburi 104:14). Eleza kwamba Mungu ndiye hukuza kila kitu. Rudia kifungu hicho pamoja na watoto.
8. Mchezo: Waonyeshe watoto tunda moja tu au mboga. Waeleze jinsi tunavyolila – kama limepikwa au kama bado bichi. Kata tunda hilo katikati na uwaonyeshe mbegu zake. Waeleze kwamba mbegu hizo zikipandwa basi matunda mengi yatakua. Tumia matunda ya aina hii: papai, embe, chungwa, hindi, na ndimu. Usitumie ndizi kwa sababu haina mbegu.
9. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya mpango wake wa kuumba vyakula.
10. **Fungua Biblia Yako katika Mathayo 13:1-8** na usimulie hadithi ya:

### VITU VINAVYOKUA

Yesu alisimulia hadithi ya mkulima aliyepanda mbegu nyingi sana. Mkulima huyu alienda shambani kwake na akaanza kupanda mbegu.

Baadhi ya mbegu hizo zilianguka karibu na njia. Hazikufunikwa na udongo. Ndege waliona mbegu hizo na wakaja wakazila zote.

Mbegu nyingine zilianguka pasipo na udongo mwingi. Zilimea kwa haraka sana. Lakini mizizi yake haikuweza kukua vizuri kwa sababu udongo huo ulikuwa na mawe. Jua lilipozuka, mimea hii iliungua na kukauka.

Mbegu nyingine nazo zilianguka penye miiba na mimea myengine. Mbegu hizi ziliota na kuanza kukua. Magugu nayo yalianza kukua. Hatimaye yalifunika mbegu hizo. Hata hazikupata nafasi ya kuendelea kukua. Mwishowe zilinyauka na kuharibika.

Hata hivyo, mbegu nyingine zilianguka katika udongo mzuri. Naye Mungu akainyesha mvua. Akaleta mwangaza wa jua. Mbegu hizi ziliota na kuanza kukua. Mwishowe zilizaa mavuno mengi.

Biblia inatuambia jinsi Mungu alivyovipangia vitu kukua. Kuna wimbo katika Biblia unaoeleza jinsi mimea hukua. Unasema hivi.

"Mungu hukuza majani.
Mungu hukuza mimea, na mwanadamu hupalilia.
Mimea huleta chakula kwa mwanadamu."

11. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
12. Waonyeshe picha namba 47. Uliza, "Ni nini kifanyacho mahindi kukua?" (mvua, jua na mbegu). "Je, ni nini kinacho kufanya ukue?" (chakula, ninapopumzika, mazoezi).
13. Mchezo: Waweza kuimba au useme tu hivi, "kichwa, mabega, magoti, vidole." (Tazama maneno yake katika somo la 41, pamoja na maagizo).
14. Wimbo: "Leo Tunafuraha"
15. Mshukuru Mungu kwa kutusaidia kukua.



Somo la 47

# VITU VINAVYOKUA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu alitupangia tupande na kuvuna.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Mungu huyameesha majani" (Zaburi 104:14).

Nyimbo:
"Jumapili Yenye Furaha"
"Dunia Ya Mungu"
"Leo Tunafuraha"

Tumia picha Namba 47.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 1:11-12, 29-30, Mwanzo 8:22; Zaburi 104:14; Mathayo 13:1-8

Ukiangalia kwa makini utaona kuwa masomo yote katika lengo hili yanaelezea muumbo wa Mungu. Somo hili laonyesha utukufu wa Mungu alipoumba mimea. Watoto wanajua jinsi mimea ikuavyo. Wasaidie ili waelewe kwamba Mungu ndiye aliyepanga hivyo.

Katika siku ya tatu, Mungu aliumba mimea na ikaota juu ya nchi. Aliumba miti na mimea mingine midogo. Baadhi ya miti huzaa matunda, na mingine haitoi cho chote. Udongo, jua na mvua husaidia mimea kuzaa matunda. Soma Mwanzo 1:11-12. Mungu aliona muumbo wake kuwa mzuri.

Mungu aliumba mimea kama chakula. Wanyama hula nyasi. Mimea mbali mbali hukua wakati tofauti katika mwaka. Mingine huhitaji mvua nyingi, na myengine huhitaji mvua kidogo tu. Mungu alimpangia mwanadamu kukuza chakula chake.

Yesu alisimulia hadithi kuhusu upandaji. Soma Mathayo 13:1-8. Alikuwa akifundisha kuhusu uenezaji wa Neno lake. Alitumia mfano wa mimea kwa sababu kila mmoja anajua kupanda, kupalilia na kuvuna.

**KULIFUNDISHA SOMO:**

1. Mkaribishe kila mtoto. Weka karibu na mlango kikapu kilicho wekwa matunda na mboga. Sema hivi mtoto aingiapo, " ________ , nimefurahi kukuona leo. Je, umeona cho chote katika kikapu ambacho wewe hupenda kula? Somo letu la leo lahusu uumbaji wa Mungu wa chakula." (Mtoto huyo asile tunda hilo, bali aseme tu lile apendalo).
2. Weka mahindi ama mboga katika chombo cha sadaka. Eleza kwamba hiyo ni njia mojawapo ya kumtolea Mungu sadaka.
3. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
4. Omba, ukimshukuru Mungu kwa ajili ya chakula.



5. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
6. Sema, "Mungu aliumba ulimwengu na kupendeza." Waonyeshe baadhi ya vifaa ulivyoleta. Waache watoto waseme kwa nini wanafikiri Mungu aliumba kila kimoja.

   Uliza, "Ni nini kinachosaidia miti na maua kukua?" (Mungu, jua, mvua). Uliza, "Je, wanyama huhitaji maji?" Je, watu nao huhitaji maji? Mungu hutuma mvua kwa sababu hutunza watu wake.
7. Kifungu cha Biblia: "'Mungu wetu, aletaye mvua' " (Yeremia 5:24). Rudia kifungu hiki pamoja na watoto.
8. **Fungua Biblia Yako Katika Wafalme wa Kwanza,** na usimulie hadithi ya:

## MVUA

"Mungu amesema kwamba hakutakuwa na mvua kwa muda wa miaka mingi. Lakini kutakuwa na mvua tu, Mungu atakaposema," Eliya akawaambia.

Eliya alikuwa akisema na mfalme Ahabu. Ahabu alikuwa amefanya mambo mengi sana kinyume cha Mungu. Mungu angezuia mvua kutonyesha.

Mvua haikunyesha jinsi Mungu alivyomwambia Eliya. Haikunyesha kwa muda miaka mitatu. Nyasi hazikukua wala mimea. Hakukuwa na chakula cha kutosha wala maji.

Siku moja Mungu alimwambia Eliya kwamba, "Nenda ukamwambie mfalme Ahabu kwamba mvua itanyesha. Nitawapatia mvua."

Eliya alipanda hadi mlimani kwenda kuomba. Aliomba na akamwambia msaidizi wake kwamba, "Tazama juu mbinguni. Je, unaona wingu lo lote?"


Eliya alimtuma msaidizi wake mara saba kwenda na kutazama kama kuna mawingu angani. Mara ya saba alirudi akiwa mwenye furaha.

Akasema, "Nimeona wingu. Lakini ni ndogo sana. Ni sawa tu na mkono wa mtu."

"Ni lazima umwambie Ahabu. Ni lazima umwambie kwamba mvua itanyesha. Mungu atatuma mvua," Eliya akamwambia.

Wingu hilo dogo liliendelea kuwa kubwa zaidi na zaidi. Kukaanza kuwa na giza. Upepo nao ukaanza kuvuma. Ukaendelea kuwa mwingi sana. Matone ya maji yakaanza kudondoka. Muda si muda yakaanza kutiririka kwa wingi na kwa haraka. Hatimaye mvua kuu ilinyesha nchini kote.

9. Maombi: Omba, "Asante sana Mungu, kwa ajili ya mvua."
10. Mchezo: Wachague watoto watatu au wanne wawe mbegu. Waambie wachuchumae chini. Mtoto mmoja atakuwa mvua. Atajifanya kuwa ananyesha. Mtoto wa tatu atakuwa jua. Atasimama huku akiwa ameshika mikono yake juu ya kichwa chake. Mvua itakaponyesha, mbegu zitaota na kukua kidogo. Mbegu zitakua pia, hata wakati jua liwakapo. Endeleeni hivyo hivyo hadi mbegu zitakapokuwa mmea uliokua kabisa.
11. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
12. Waonyeshe picha namba 45 na ueleze kuhusu mvua na mahindi.



Somo la 46

# JUA

**KULITAYARISHA SOMO NYUMBANI:**

**Mkazo wa Somo:** Mungu huleta jua ili tupate mwangaza na joto.

**Kifungu cha Kukumbuka:** "Baba yenu aliye mbinguni...huwaangazia jua lake" (Mathayo 5:45)

Nyimbo:
"Jumapili Yenye Furaha"
"Dunia Ya Mungu"

Tumia picha Namba 46.

**Kujitayarisha kwa Mwalimu na Somo la Biblia:** Mwanzo 1:14-19; Zaburi 74:16; Zaburi 104:19, 22-23

Vifungu hivi vyote vyaeleza kuhusu jua. Mungu anauwezo juu ya viumbe vyake. Aliumba jua ili litenganishe usiku na mchana. Mwanadamu hufanya kazi jua liwakapo. Yeye hulala wakati wa usiku. Haya yote ni mpango wa Mungu.

Mungu alitumia hekima yake kwa kuumba jua na mwezi. Kuna masaa kumi na mawili ya kuona mwangaza na masaa kumi na mawili ya kuwa na giza. Mwanadamu huamka kunapopambazuka. Lakini kunapokuchwa, yeye huenda kupumzika.

Mungu ni mwenye uwezo. Aliumba na pia anatawala muumbo wote. Mungu anao hekima. Alimpangia mwanadamu kufanya kazi na pia kupumzika. Mwanadamu hupanda mbegu. Naye Mungu hutuma mvua na jua. Mimea hukua, nayo hutoa mazao.

1. Wakaribishe watoto kwa kusema, "Leo nina furaha sana, kwa sababu ——— (sema jina la mtoto) amehudhuria Shule ya Jumapili."
2. Sadaka: Watoto watatakiwa kuweka sadaka katika chombo cha sadaka mara tu wafikapo darasani.
3. Wimbo: "Jumapili Yenye Furaha"
4. Kutembea: Simameni katika mstari. Mwaweza kusimama katika mistari miwili kama una zaidi ya watoto kumi. Tembeeni mkienda nje. Taja majina ya vitu ambavyo vinakua. Hakikisha umeongea kuhusu kivuli cha mti. Je, ni kirefu? Uliza, "Mwasikia baridi au joto? Je, nini kinachowafanya kusikia joto? (Jua). "Je, ni nani aliyeumba jua?" (Mungu). Sasa rudini darasani.
5. Wimbo: "Dunia ya Mungu"
6. Kifungu cha Biblia: Waambie watoto wachague alama uliyoweka katika Biblia. Soma kila kifungu. Tumia vifungu vitano vya lengo la somo hili. Mwanzo 1:5, Yeremia 5:24, Mathayo 5:45, Zaburi 104:15, Mhubiri 3:11.



7. **Fungua Biblia Yako katika Zaburi 104** na usimulie hadithi ya:

**JUA**

Mungu aliumba kila kitu. Aliumba nchi. Akaumba anga na wanyama. Aliumba pia, mwezi na nyota na hata jua.

Mungu alikuwa na kusudi maalum la kuumba kila kitu. Jua ni kubwa na hutoa mwangaza. Sisi hupata nuru linapotoa mwangaza. Nuru hutusaidia kuona jinsi tufanyavyo kazi. Kusingekuwapo na nuru, basi tungeishi katika giza. Hatungeweza kucheza wala kuona kazi tufanyayo.

Jua husaidia mbegu kukua. Mbegu huhitaji udongo, maji na mwangaza wa jua. Sisi hupanda mbegu kabla ya mvua kuanza. Mvua husaidia mbegu kukua. Lakini ni lazima zipate mwangaza.

Jua hutoa joto. Nchi hupata joto hili. Hata nasi pia husikia joto hili. Hebu fikiria kuhusu usiku wenye baridi sana. Kuna giza na pia unasikia baridi. Hatimaye kunakucha. Na jua nalo limetoa mwangaza. Hapo huamka kutoka kitandani na kwenda kuota jua. Jinsi uendeleavyo kusimama katika jua ndivyo unavyo zidi kusikia joto zaidi na zaidi. Mwishowe huwa husikii baridi tena. Basi tumshukuru Mungu kwa kuumba jua litupalo joto.

Jua hufanya kazi ambayo sisi huiona. Jua hukausha maji ya mvua kutoka ardhini. Kama kusingekuwa na jua basi maji ya mvua yangekuwa juu ardhini. Hata maji hayo yangeweza kuwa mengi na mengi zaidi.

Kama kusingekuwa na jua, basi nguo zilizolowa hazingeweza kukauka, joto la jua hukausha nguo.

Tunashukuru sana kwa sababu Mungu aliumba jua. Hasa jua hutusaidia kwa njia nyingi sana.

8. Maombi: Mshukuru Mungu kwa ajili ya jua.
9. Vifungu vya Wimbo:

Mwalimu sema, "Ah, nani awezaye kulifanya jua liangaze?"
Watoto wajibu, "Siwezi nikalifanya jua liangaze."
Mwalimu sema, "Ah, nani awezaye kulifanya jua liangaze?"
Watoto wajibu, "Hakuna ye yote ila Mungu tu ndiye awezaye kulifanya jua liangaze."

10. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
11. Kutembea: Nendeni kutembea nje tena. Hakikisha mmeona kivuli cha mti. Je, wakati huu kimekuwa kifupi? Waeleze watoto kwamba hii ni mojawapo ya njia za kujua saa. Wakati wa saa sita za mchana, kivuli cha mti kitakuwa chini yake. Wakati wa jioni kivuli hicho kitakuwa kirefu. Pia, kitakuwa sehemu ya pili ya mti huo.
12. Maombi: Omba, "Asante sana Mungu kwa ajili ya vitu vyote vya kupendeza ulivyoumba."
13. Wimbo: "Dunia Ya Mungu"
14. Waonyeshe picha namba 46. Waambie majina ya vitu vilivyomo katika picha hiyo ambavyo viliumbwa na Mungu: jua, miti, nyasi, milima, na kadhalika.